# ELIMU

# YA

# KUHUBIRI

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha ELIMU YA KUHUBIRI. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

ELIMU YA KUHUBIRI.

1.Kuhubiri ni nini?…………………………………………………..

2. Habari njema……………………………………………………..

3. Kutubu……………………………………………………………….

4. Ufalme wa Mungu……………………………………………….

5. Muujiza wa ufufuko wa Yesu……………………………….

6. kuokoka……………………………………………………………..

7. Yesu ni Masihi au Kristo………………………………………

8. Kumcha Mungu…………………………………………………..

9.Kitabu cha Mhubiri……………………………………………….

10.Biblia…………………………………………………………………

11.Mtumishi wa Yesu………………………………………………

12.Tajiri…………………………………………………………………

13.Mhubiri……………………………………………………………

14.Upako au Roho Ya mhubiri………………………………….

15.Ujira wa kuhubiri………………………………………………..

16.Kuokoka…………………………………………………………….

16. Mwisho……………………………………………………………..

## 1. KUHUBIRI NI NINI?

**Kuhubiri** ni kutoa **habari njema** za Yesu mfufuka kwa wenye dhambi wapate kuokoka yaani wenye dhambi wanabadilishwa na Yesu kwa kutubu,kubatizwa na kujazwa Roho Mtakatifu ndio kuokoka hivyo wanapewa haki ya maisha ya Yesu na kuacha maisha yao ya dhambi.

**Isaya 45 : 21** "**Hubiri**ni, **toeni habari**; naam, na wafanye mashauri pamoja; ni nani aliyeonyesha haya tangu zamani za kale? Ni nani aliyeyahubiri hapo zamani? Si mimi, Bwana? Wala hapana Mungu zaidi ya mimi; Mungu mwenye haki, mwokozi; hapana mwingine zaidi ya mimi. "

Habari njema aliyohubiri Yesu kwa wenye dhambi ni ya ktk

**Marko 1: 14 — 15** "Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya, akiihubiri **Habari Njema** ya Mungu,

akisema, **Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni**, **na kuiamini Injili.** "

Habari inataka mwanadamu mwenye dhambi atubu na kuamini injili ndipo anapata kuokoka. Habari hii huweza kutumiwa wahubiri ya Yesu kuwahubiri wenye dhambi waokoke kwa jina la Yesu.

**Yoh 16 : 13** "..., lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo **atawapasha habari yake**. " Ili roho mtakatifu akupashe habari njema ni lazima ushirika wako na Mungu uwe mzuri hasa kwa wahubiri ili upate habari njema mpya zitokazo kwa Yesu za kuhubiri injili.**Kuhubiri** ni kusema maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu wenye dhambi wapokee **Imani ya kuokoka** ya Yesu mfufuka kama alivyosema ktk aaminiye injili ya Yesu na kubatizwa **ataokoka.**

**Marko 16:15—16** " Aaminiye na kubatizwa **ataokoka**; asiyeamini, atahukumiwa. "

# 2.HABARI NJEMA

**Habari njema** ya Mungu ni ile aliyohubiri Yesu ktk **Marko 1 : 14 –15**

**"** Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya, **akiihubiri Habari Njema** ya Mungu, akisema, **Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili.** "

Habari hiyo njema kwa wakati wetu **wahubiri** wanaomfuata Yesu walipaswa kuihubiri kwa wenye dhambi wapate kuokoka. Ktk habari njema wanapoihubiri kwa wenye dhambi muujiza wa mungu alioutenda kwa mwanaye Yesu ni muhimu kuhubiriwa na kufundishwa kwa wenye dhambi ndio ulioleta upatanisho kati ya mwanadamu na mungu ni jibu la kifo ndio uliosababisha ufalme wa mungu kuja duniani yaani roho mtakatifu kushuka kwa watubuo kwa jina la yesu na waokubali kubatizwa kama yesu na kuokoka Lakini pia yesu alipoihubiri hiyo habari njema aliponya wagonjwa na udhaifu wa kila namna **Mhubiri** akihubiri hiyo habari njema Yesu angelimtumia kuponya wagonjwa na udhaifu wa kila namna. **Mathayo 4:23**

**Rumi 10 : 9** "Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, **utaokoka.** "

**Rumi 10 : 13 – 16** "kwa kuwa, Kila atakayeliitia Jina la Bwana **ataokoka.** Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo **mhubiri**? Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio **habari ya mema**! Lakini si wote walioitii ile **habari njema.** Kwa maana Isaya asema, Bwana, ni nani aliyeziamini habari zetu? "Maandiko hayo hapo juu yanathibitisha Mhubiri amepewa na yesu kuihubiri habari njema moja tu aliyoihubiri Yesu ambaye baada ya kufufuka anataka waokoke. Wapo manabii na mitume nao hutumiwa Yesu kufanya kazi ya kuhubiri wenye dhambi aliyotumwa Yesu na Mungu yaani baba yake.

# 3. KUTUBU

Kutubu ni kuacha maisha ya dhambi na kuishi maisha ya haki. Kutubu ni kuacha kutenda mabaya na kutenda mema. Kutubu ni kumgeukia mungu na kuacha kuwa shingo ngumu. Mfano wa dhambi ni kupokea rushwa na wa haki ni kumwabududu Yesu na Baba yake na kutoabudu sanamu ambazo nyingi ni kazi za mikono ya waki.

Kutubu ni sehemu ya ile habari njema aliyoihubiri Yesu kwa wenye dhambi . Sehemu hii ya habari alipowaagiza **mitume** ilithibitishwa kwa ishara ya kutoa pepo. **Mitume** wakibubiri kutubu wakimfuata Yesu hutumiwa naye kutenda matenda matendo makuu ya mungu.

**Marko 6 : 12—13**

"Wakatoka, wakahubiri kwamba watu watubu. Wakatoa pepo wengi, wakapaka mafuta watu wengi waliokuwa wagonjwa, wakawapoza. "

Kutubu kukihubiriwa na mitume roho mtakatifu huthibitisha kwa ishara.Wenye pepo hutolewa pepo kwa jina la yesu na wagonjwa hupozwa kwa kupakwa mafuta yaliyombewa.

**Warumi 2: 21 - 22** " basi wewe umfundishaye mwingine, je! Hujifundishi mwenyewe? Wewe uhubiriye kwamba mtu asiibe, waiba mwenyewe? Wewe usemaye kwamba mtu asizini, wazini mwenyewe? Wewe uchukiaye sanamu, wateka mahekalu? "

Ukihubiri watu wenye dhambi kutubu dhambi fulani mfano kuiba **Mhubiri** unayeubiri hutakiwi kuwa hatia yaani kwa mfano huo na wewe usiwe mwizi au usiwe na tabia ya wizi.

**Mhubiri** unakiwa kujihubiria mwenyewe kabla ya kuwahubiri wengine ili upate kujitoa boriti iliyo ndani yako kabla kuona boriti iliyo kwa wale unaoenda kuwahubiri watubu. Kisha kuokoka.

## 4. UFALME WA MUNGU UMEKARIBIA

Ufalme wa mungu ni utawala wa mungu ambao mungu yaani Baba yake Yesu ni mfalme na Yesu ni mwana na mfalme kwa wenye mwili

Waliokokoka na wenye roho yake yaani roho mtakatifu msaidizi. Na upo juu kuliko tawala yoyote ktk ulimwengu wa roho na mwili pia.

Yesu aliwafundisha **mitume** kuhubiri Ufame wa mungu umekaribia kama sehemu ya habari njema aliyoihuiri yeye na aliwaamuru kutenda matendo makuu ya mungu kama kutasa wakoma.

**Mathayo 10**

"Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema, **Ufalme wa mbinguni umekaribia.**

Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure. "

**Mathayo 4:17**

"Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, Tubuni; kwa maana **ufalme wa mbinguni umekaribia.** "

Habari njema aliyohubiri yesu ndio juu ufalme wa mungu umekaribia na ufalme wa mbinguni umekaribia una maana moja au iliyokaribu sawa.

Ni **mitume au wahubiri** wakihubiri hiyo habari njema kwa watu hutumiwa na mungu kuponya wagonjwa wakimfuata yesu .

**Mitume** hutuiwa na Yesu kutoa pepo na kupoza wagonjwa kwa kuwapaka mafuta wanawahubiri watu **watubu** yaani nusu habari ya habari njema na kupoza wagonjwa,kufufua wafu,kutakasa wakoma na kutoa pepo wanapowahubiria watu **ufalme wa mbinguni umekaribia** na hii ni nusu habari ya ile habari njema ambayo ikutukiunganisha na ile nusu habari ya kwanza tunapata habari njema kamili

## 5. MUUJIZA WA UFUFUKO WA YESU

Kuna kuhubiri kwa kusema muujiza wa ufufuko wa Yesu na umuhimu wake kwa wenye dhambi . Jinsi Yesu alivyo jibu la kifo kwa mwanadamu . Mtu hawezi fufuka isipokuwa ameishinda dhambi ktk maisha yake alipoishi duniani ni yesu ni tu ndio aliweza wengine tunarithi haki ya maisha yake ya haki alipokuwa ktk dunia. Dhambi ilileta kifo na haki ilileta uzima.

**Matendo 17:18** " Na baadhi ya Waepikureo na Wastoiko, wenye ujuzi, wakakutana naye. Wengine wakasema, Mpuzi huyu anataka kusema nini? Wengine walisema, Anaonekana kuwa mtangaza habari za miungu migeni, kwa maana alikuwa akihubiri **habari za Yesu na ufufuo.**

Ni mhubiri,mwalimu na mtume Paulo alihubiri kwa wenye dhambi muujiza wa ufufuo wa Yesu na umuhimu wake ushirika kati ya mungu na mwanadamu ktk maisha haya na baada ya maisha haya unakufunulia ukimfuata utakwenda kuzuri utarudi ktk dunia baada kifo kisha atachukua na kukupeleka ktk makao ya mbinguni au utapaa naye juu hadi ktk makao ya mbinguni. Muujiza wa ufufuko wa Yesu unapa ufahamu kile mungu atakachotenda kwako baada siku tatu atakufufua kama alivyotenda kwa Yesu ikiwa ulikuwa uliyeokoka uliyekufa. Nawe utapaa na kupelekwa makao ya mbinguni aliyoindaa Yesu hilo ndilo tumaini la mtu aliyeokoka kabla ya hajafa.

**Marko 5.** "'..Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu, **kawahubiri** ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu. Akaenda zake, akaanza **kuhubiri** katika Dekapoli, ni mambo gani makuu Yesu aliyomtendea; watu wote wakastaajabu. .."

Kuna kuwatuma wale walotedewa na mungu na kuokoka kwenda kuwahubiri wale waliowashuhudia ukiwa na tatizo lililotatuliwa na Yesu au Baba yake yaani mungu. Mfano umetendewa muujiza ktk biashara yako unapata faida pengine ulitaka kufunga kutoka na kutopata faida mbali kutumia elimu yako pengine elimu ya biashara uliyosomea. Na wafanyakazi wako wa karibu wanafahamu au wafanyabiashara wenzako wanaelewa mambo kwako hayaendi sawa.

Mhubiri ukimfuata Yesu kwa habari ya wale wanaotendewa na mungu anatakiwa kutuma wakahubiri jamaa ,rafiki na jirani zao.

# 6. KUOKOKA

Kuna kuhubiri kuokoka  kwa wenye dhambi kwa hekima. Mhubiri wa injili unamfundisha mwenye dhambi maana ya kukokoka na yale mabadiliko ya kiroho yanatokea ndani yake wakati anapomkiri Yesu kama Bwana mwokozi.Unamfundisha ajue ukweli wa Mungu au Baba Yesu anachotenda ktk Roho yake na mwili wake kwa sehemu wakati unapomkiri Yesu kama Bwana na Mwokozi wa Maisha yako kutoka ktk dhambi. Mambo atakayokutendea mungu hutukia kufumba na kufumbua mfano  kuhamishwa ktk roho kutoka kumilikiwa na nguvu za giza na kuingizwa ktk ufalme wa mbinguni ambao ni wa nuru na wa haki., Dalili za ufalme wa mungu kuwa umeingia ndani yako au ktk maisha yako furaha,amani,haki na upendo,kunena kwa lugha, Mamlaka anayowpewa na Mungu,Nguvu za Roho mtakatifu,

Sauti ya Mungu yenye kushushudiwa na roho mtakatifu na yenye Msukumo.,Kuzaliwa kwa roho yako. Na kuonekana mbinguni mbele Baba (Maombi). Nuru kuingia ndani ya maisha yako kwa Yesu ni nuru maisha yako kuvikwa haki ya Yesu. Kuomba na kujibiwa  haja ya moyo wako na  uwe mtu wa shukrani na mwenye kukaa mbali na dhambi na kumtumikia Yesu kwa kutii neno lake lilimo ktk vitabu vya injili vya Biblia (Marko, Mathayo,Yohane,Marko),au kupitia watumishi wa Mungu . Wengine wanapewa neema ya kusikia sauti ya Mungu,Yesu na Roho mtakatifu kwa ajili ya kuwaongoza ktk matakwa na kusudi lake.

**Rumi 10** :“ Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, **utaokoka.** “ kwa kuwa, Kila atakayeliitia Jina la Bwana **ataokoka.** ,Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo **mhubiri?** “

Mhubiri ni mtumishi ws Yesu mwenye kszi ys kuhubiri kuokoks kws jina la Yesu kwa wenye dhambi kwa hekima na nguvu.

## 7. MAOMBI YALIYO MAPENZI YA MUNGU

Maombi yaliyo mapenzi ya mungu kwa wahubiri wa injili kwa wenye dhambi ili waokoke ni kudumu ktk :

1) .Kuwaombea wenye dhambi Yesu aliokusudia kupitia wewe yaani mhubiri waokoke ktk siku za maisha na utumishi wako uliopewa na Yesu kulingana neema aliyoweka mungu yaani Baba yake Yesu ndani yako.

**Rumi 10: 1**

“Ndugu zangu, nitakayo sana moyoni mwangu, na dua yangu **nimwombayo** Mungu, ni kwa ajili yao, ili **waokolewe.** “

2).Kuomba uokolewe na wasioamini na makosa yanayoweza kuleta taabu ktk utumishi wako.

3).Kuomba uokolewe na taabu.za wengine yaani kutoingizwa ktk taabu za wengine.

**Yohane 4.:8**

“Mimi naliwatuma myavune yale **msiyoyataabikia;** wengine **wali taabika,** nanyi mmeingia katika **taabu** yao.”

4) .Kuomba roho mtakatifu akuongoze ktk kweli ili Yesu akuweke huru mbali na dhambi uwe mwana wa mungu. Ufikie utukufu wa maisha yasiyo na dhambi kama ya Yesu. Ya kushuhudiwa na mungu na watu pia.

**Yohane 8.”6** “Ni nani miongoni mwenu **anishuhudiaye ya kuwa nina dhambi?** Nami nikisema kweli, mbona ninyi hamnisadiki? “

5).Kuwaombea waokokao kudumu na ktk imani ya Yesu na kuleta wengine kwa Yesu.

**Yohane 15.16 “**Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae **matunda;** na **matunda** yenu yapate kukaa; ili kwamba lo lote mmwombalo Baba kwa jina langu awapeni. “

## 8. YESU NI MASIHI AU KRISTO

Kuna kuhubiri Yesu ni Masihi au Kristo. Kuhubiri huko kulifaa sana kwa waisraeli walioshindwa kumtambua Yesu kuwa ndiye kristo waliyeahidiwa na Mungu kuwa angekuja kuwakoa kutoka ktk dhambi na kuwa mfalme wao mwenye nguvu na mshauri mwenye kutatua matatizo yao ambao wakati huo jamii yao ilikuwa maskini na ilikuwa inatawaliwa kwa sehemu. Ambaye alikuja na wakamtendea kama manabii wao walivyosema.

Kuhubiri Yesu ni Masihi au kristo kwa faa sana waisraeli ambao mpaka leo wanamsubiri Masihi au kristo na wenye imani hiyo ya kumsubiri kristo au masihi.Yesu baada ya waisraeli hasa mafarisayo,waandishi na masaduka kuingiwa na ugumu wa moyo juu yake kuwa ni kristo waliyeahadiwa aliwaambia ukweli wanafunzi wake ambao ni mitume kumi na mbili kuwa yeye ndiye kristo au masihi na watatokea makristo wa uongo baada yeye kukataliwa na waisraeli watakao wadanganya waisraeli wasiomwami kuwa ndiye na hata baadhi ya waisraeli waliomwamini watadanganyika na kuiacha imani ya kweli. Mfano **Matendo 5:34 — 39**

" ….Kwa sababu kabla ya siku hizi aliondoka **Theuda,** akijidai ya kuwa yeye ni **mtu mkuu,** watu wapata mia nne wakashikamana naye; naye aliuawa na wote waliomsadiki **wakatawanyika** wakawa si kitu. Baada ya mtu huyo aliondoka **Yuda Mgalilaya,** siku zile za kuandikiwa orodha, akawavuta watu kadha wa kadha nyuma yake, naye pia **akapotea** na wote waliomsadiki **wakatawanyika**. Basi sasa nawaambia, Jiepusheni na watu hawa, waacheni; kwa kuwa shauri hili au kazi hii ikiwa imetoka kwa **binadamu, itavunjwa**, lakini ikiwa imetoka kwa **Mungu hamwezi kuivunja;** msije mkaonekana kuwa **mnapigana na Mungu.** "

# 9. KUMCHA MUNGU

Kuna kuhubiri kumcha Mungu ambako kwa faa sana unasema kabila juu ya uovu wao au taifa juu ya uovu wao mfano makabila ya wafugaji kama wamasai juu ya ukeketaji au taifa kama Nigeria juu ya rushwa au india,china,Thailand, juu ya sanamu za kuchonga au kufinyangwa za michanga ya rangi , silva na shaba.

**Ufunuo wa Yohana 14 : 6—7**

"Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, **awahubiri** hao wakaao juu ya nchi, na kila **taifa** na **kabila** na **lugha** na **jamaa,**

akasema kwa sauti kuu, **Mcheni Mungu,** na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji. "

Kumcha mungu ni kuchukia uovu mfano kiburi ,majivuno na njia mbovu.Kuhubiri kumcha mungu kwa kabila au taifa ni kuwapa habari kuchukia uovu fulani wa kabila lao au taifa lao ambao viongozi vipofu wa kabila husimamia utekelezwe ktk kabila lao hawaoni kasoro./ubatili.

Kuhubiri kumcha mungu kwa jamaa (ndugu,Ukoo,familia) ni kuwapa habari kuchukia uovu fulani wa jamaa (ndugu,Ukoo,familia) yako ambao ni chukizo kwa Baba yake Yesu ,Yesu na Roho mtakatifu.

**Mhubiri** Yesu au roho mtakatifu anapokupeleka kwenda kuhubiri kabila au taifa liokoke ili kutoka ktk uovu fulani wa kutoka ktk uovu fulani wa kikabila au Taifa unatakiwa kuwahubiri kumcha mungu kisha uwahekimishe kwa kifupi kuokoka na kuwaita waliotayari kwa kuokoka.

# 10. KUHUBIRI KITABU CHA MHUBIRI

Kuna kuhubiri kwa kutumia kitabu cha mhubiri na kumfuata yesu anachotaka kwa wenye dhambi ni kuokoka. Ukisoma kitabu cha macho ya kiroho ya kihuduma za kanisa hasa ile ya mhubiri ataona kitabu kimeandikwa watu wenye dhambi wanatakiwa kuhudumiwa ili waokoke kwa kuwahubiria waokooke.

Zipo njia kadhaa kuhubiri kitabu cha mhubiri nao ni kama zifuatazo:

1) Kuomba watu wote walioandikwa ktk kitabu cha mhubiri wenye dhambi mungu awelete ktk mkutano wa injili na kuwahubiri habari njema ya mungu au Yesu na ufufuo na kuwaita kwa kumkiri yesu kama Bwana na mwokozi yaani kuokoka. Mfano Maskini,mtenda mema na dhambi,Tajiri mgonjwa,Mpokea Rushwa aliyearibikiwa ufahamu, Matusi,Uvivu kwa wafanyakazi wa tawala za dunia.Anasa,Washerati Lakini pia kuna Mcha mungu n.k
2) Kusoma ukweli mtu aliye ktk kitabu cha mhubiri mfano wa wenye dhambi kuhubiri injili kwa mtu au watu wenye dhambi waokoke. Mfano Mtenda mema na dhambi au Kiongozi wa nchi anayeona maskini anaonewa asiyechukua hatua au wenye kuzivunja amri za mungu na mwenye hofu ukifa aona giza kwa habari kifo.
3) Mhubiri wa Yesu ukitaka Kuhubiri Kwa kutumia Kitabu cha mhubiri na Lazima ukichanganye na vitabu vya inji li (Mathayo,marko,luka,Yohana) ndipo utakapowahubiria injili watu wenye dhambi waokoke. Roho mtakatifu na akusaidie upate ufahamu juu ya hayo niliyokuandikia kama upako a ujazo wa roho mtatifu kupita wengine waliokoka wa kuwahubiria wenye dhambi waokoke ukawe mkamilifu kt utumishi wako kwa Yesu na Roho mtakatifu ktk kumtii wakupelekapo. Ndipo mungu hatakupungukia kwa riziki na maisha yako yatakuwa na heri wala siyo ole.

# 11.BIBLIA

Kuna kuhubiri kwa kutumia Biblia . Mhubiri na mtumishi wa Yesu uliyeokoka unayependa kuhubiri kwa kutumia biblia ni kutumia mistari ya maandiko yenye neno **kuhubiri tu** ktk Biblia Na yesu atukumia sawa neema na karama za roho mtakatifu alikupa mungu yaani Baba yesu kujidhihirisha yeye na Baba yake kwa nguvu na dalili za roho mtakatifu kwa watu wasioamini na wenye dhambi.

Mfano wa mistari ya maandiko ktk biblia agano la jipya ni ifuatayo

**Mathayo 4:17**

"Tokea wakati huo Yesu alianza **kuhubiri,** na kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. "

**Marko 3:14**

"Akaweka watu kumi na wawili, wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume **kuhubiri,** "

**Luka 4:18**

Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta ku**wahubiri** maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa,

**Matendo 3.18 "**Lakini mambo yale **aliyohubiri** Mungu tangu zamani kwa kinywa cha manabii wake wote, ya kwamba Kristo wake atateswa, ameyatimiza hivyo. "

Mfano wa mistari ya maandiko ktk biblia agano la Kale ni ifuatayo

**Kutoka 17: 14** Bwana akamwambia Musa, Andika habari hii katika kitabu iwe ukumbusho, kisha **ihubiri** masikioni mwa Yoshua; ya kuwa nitaufuta ukumbusho wa Amaleki kabisa, usiwe tena chini ya mbingu.

## 12. MTUMISHI WA YESU

Kuna kuhubiri mtumishi wa Yesu au mungu yaani Baba yake Yesu

Anayekuja nyuma yako ni mkubwa na wanapaswa kanisa au watu wenye dhambi waliokudiwa na mungu kumpokea. Baada roho mtakatifu kukupasha habari kupitia maombi ya mfungo wa muda mrefu.

Mtumishi wa Yesu anayekuja Nyuma Yako aliyetumwa na Yesu anaweza kuwa ni mtume, nabii, mwandishi ,Mchungaji,Mwalimu na Mwinjilisti n.k Huo ndio ukweli wakati wetu.

**Mathayo 3.11**

Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba; bali yeye **ajaye nyuma yangu** ana nguvu kuliko mimi, wala sistahili hata kuvichukua viatu vyake; yeye atawabatiza kwa **Roho Mtakatifu** na kwa moto.

Mhubiri anayehubiri mtumishi wa Yesu anayekuja nyuma yako ni vizuri kama ushirika wako na mungu ni mzuri kukesha ktk maombi kama agizo la yesu kwa watumishi wake wasilale usiku wawe kama yeye na kumuuliza mungu akupashe habari njema ya ujio wa mtumishi wa mungu nyuma yako kwa kumtumia roho mtakatifu aliyetumwa au pelekwa na Mungu au Yesu.

Kukaa Ktk Maombi kutakupa kufahamu mtumishi ajaye nyuma yako na kusema na Mungu ni wa ile neema ya utumishi aliuweka Mungu ndani yako yaani ni miongoni mwa watu watakaookoka ktk utumishi wako au wataokoka nje ya utumishi wako. Mtumishi ajaye nyuma yako ni mkubwa sio mwenye kupewa upako au ujazo wa roho mtakatifu kupita wengine waliokoka kwa kusudi la kuwahudumia kanisa au wenye dhambi waliokusudiwa kuokoka.

Kukaa na Roho mtakatifu ktk akufundishe wale unaowahubiri injili waokoke wafanyeje ili wapate kumpokea ajaye nyuma yako na kutii yale atakayosema nao ya kuwa ni ya mungu yaani Baba yake Yesu aliyeumba watu (jina lake NIKO AMBAYE NIKO).

## 13. TAJIRI

Kuna kuhubiri amri za mungu na mema kwa tajiri au mfanyabiashara.Amri hizo ni usiue, usiibe na kutamani mali ya watu wengine, shika sabato,usizini na kutamani mke wa jirani yako, kuheshimu wazazi wako na mfano wa mema ni kama akopaye kwako usitarajie akulipe ikiwa sehemu ya pesa ya akiba pengine na imebaki baada ya kumkopesha; kutengeza shule au hospitali vijijini ktk vijiji visivyo na huduma za kijamii kama hizo; kutengeneza jengo la kanisa au Mkutano wa injili na kuomba ktk kanisa la waliokoka mtumshi aliye tayari na mwenye kutamulika na kanisa kwenda kuhudumia ktk vijiji ambapo huduma ya kanisa ya waliokoka haipo.

**Mathayo 19 : 17 — 22**

1) **Amri za Mungu (Kumcha Mungu)**

"Akamwambia Kwani kuniuliza habari ya wema? Aliye mwema ni mmoja. Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike **amri.** Akamwambia, Zipi? Yesu akasema, Ni hizi, **Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo, Waheshimu baba yako na mama yako, na, Mpende jirani yako kama nafsi yako.**

**2) Kutenda Mema**

Yule kijana akamwambia, Haya yote nimeyashika; nimepungukiwa na nini tena? Yesu akamwambia, Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda **ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni;** kisha njoo unifuate. Yule kijana alipolisikia neno lile, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi. "

Kwa habari ya kuuza vyote ulivyo navyo na kuwapa maskini kama yako ya kutenda mema pengine ulikuwa utendi mema kila mungu alipokuletea mtu wa kutenda mema mfano wa Yesu wa yule tajiri na lazaro maskini lakini inawezekana wewe ni mtumishi wake kama mitume ila mali ndio kikwazo cha kumtumikia mungu

## 14. MHUBIRI

**Mhubiri** ni mtumishi wa Yesu anayehubiri habari njema ya mungu au injili kwa wenye dhambi ili waokoke na maisha ya dhambi kwa kumwani Yesu kama Bwana na Mwokozi wa maisha yao. Habari hiyo njema ya mungu nimeiandika ktk sura ya pili ya kitabu hiki na injili anayotakiwa kuhubiri kwa wenye dhambi ni muujiza wa ufufuo wa Yesu aliotenda mungu kwa Yesu ni jibu tosha juu ya mswali ya mwanadamu kuhusu kifo . Mwanadamu mwenye dhambi amwamini nani atakwenda kuzuri baada kufa ktk wale aliowatuma mungu au wanaozungumzia kifo? Na maamuzi hayo mwanadamu anatakiwa kuyafanya akiwa duniani kabla hajafa kama mtii mungu ktk kazi na ndoa au kuoa ni mwenye kumaanisha kimatendo na yu hodari hali kadhalika ktk kifo mfano na kumtii yesu kwa kutenda yaliyo ktk injili aliyosema Yesu au kama umepewa neema ya kusikia sauti ya neno lake au sauti ya roho mtakatifu ikuongozayo ktk utumishi uliowekwa ndani yako au kupitia watumishi wa mungu ambao Yesu anasema nao au njia kusoma na kutafakari yaliyomo ktk biblia kwa kufundishwa na kuongozwa na roho mtakatifu baada ya kuokoka.

**Mhubiri** ni moja ya huduma za kanisa la waliokoka yenye kuwapatia wenyeji wa ufalme wa mbinguni wenye dhambi waokokao na kulizidisha kanisa .

**Mhubiri** hushirikiana na Yesu kwenda kutafuta mwenye dhambi aliyepotea ambaye tangu kuumbwa kwa ulimwengu alichaguliwa Mungu afanane na Yesu ila wakati ulipowadia akafunuliwa ni mwana kwa kuokoka baada ya kuhubiriwa injili na kuipokea.au kuikubali kwa moyo.(Kuamini maana yake kukubali kwa moyo)

**Mhubiri** ni mtumishi wa yesu anapelekwa na Bwana yesu au Roho Mtakatifu Msaidizi kuhubiri kuokoka kwa hekima na nguvu kwa wenye dhambi ili wamwamini yesu kama Mfalme,Bwana na Mwokozi

# 13. UPAKO AU ROHO YA MHUBIRI

Upako wa Mhubiri au roho ya Mhubiri aliyepelekwa na Yesu au roho mtakatifu una sifa zifuatazo kwa filipo na Paulo kama wahubiri wa injili tunaweza jifunza kwa sehemu:=>

1) Hekima
2) Amri ya kutoa pepo
3) Kuponya wagonjwa
4) Mijiuza.

Sika ya kitabia inayohitajika: =>

1) **Kumcha Mungu**

Ni kuchukia uovu, Ni msingi wa hekima na uponyaji.

**2) Mwema**

Ni kuwaveka wenye dhambi walio uchi nguo kwa kuwahubiria waokoke.

Ushirika wa Mhubiri na mungu ktk kazi ya kuhubiri injili:=>

1) **Yesu**

Wanapewa neema ya kumwona na kusikia sauti yake Yesu akiwa juu ya dunia baada ya mbingu kufunguka na kutoa agizo mara kwanza Kwa wahubiri au walimu ndio wanalotakiwa kulitekeleza ktk maisha yako yote.

**2)Roho mtakatifu**

Sauti ya roho mtakatifu ya kukupeleka kuhubiri injili ya yesu kwa wenye dhambi unapokaa na mungu ktk maombi ya kiutumishi na kumuuliza pengine juu ya kazi yake

**3)Malaika** “Sauti ya malaika ikikuongoza ktk kazi ya kuhubiri injili ya yesu Mfufuka kwa waliokusudiwa kuokoka na Mungu mwenye kutoa neema”

## 14. UJIRA WA KUHUBIRI

**Mathayo 10** " .. Hao Thenashara Yesu aliwatuma, akawaagiza, akisema, Katika njia ya Mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie. Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. Na katika kuenenda kwenu, **hubirini,** mkisema, **Ufalme wa mbinguni umekaribia.** Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure. Msichukue dhahabu, wala fedha, wala mapesa mishipini mwenu; wala mkoba wa safari, wala kanzu mbili, wala viatu, wala fimbo; maana mtenda kazi astahili **posho lake**. ,,,"

Ktk andiko la hapo juu yesu alituma Thenashara ambao ndio mitume kumi na mbili kwenda kufanya kazi ya **kuhubiri** na kuwaahadi ktk hiyo kazi ujira wake ni **posho.** Kwa wakati wetu posho ni pesa au fedha anayolipwa kibarua kwa siku kwa ajili ya chakula na mahitaji madogo mfano nauli ya kibarua.

**1 wokor 9 : 13—14** "Hamjui ya kuwa wale wazifanyao kazi za hekaluni hula katika vitu vya hekalu, na wale waihudumiao madhabahu huwa na fungu lao katika vitu vya madhabahu? Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale **waihubirio Injili** wapate **riziki** kwa hiyo Injili. "

Ujira wa kazi ya kuhubiri ni **riziki** kwa **wahubiri**. Wahubiri wanapopelekwa na Yesu au Roho mtakatifu kuwahubiria injili wenye dhambi waokoke watachovuna cha mwilini kutoka kwa wanaikubali injili yao ni **Riziki ni** chakula cha siku nzima mfano **mkate.**

Kwa **mitume** ni **posho** ndio ujira wa kazi ya kuhubiri lakini kwa **wahubiri** ni **riziki** ndio ujira wa kazi ya kuhubiri na Nabii ni **riziki** ndio ujira wa kazi ya kuhubiri kwa kutoa unabii akitumwa mungu . Na riziki hutoka kwa Baba wa mbinguni hata waliokoka wasalipo sala aliyofundisha mitume na wafuasi kusali kila siku Baba wa mbinguni huwapa **riziki** kama sehemu ya hiyo sala.

## 13. ADUI YAKO KTK KUHUBIRI

Wapo adui ktk kazi ya kuhubiri injili kwa wenye dhambi.

Mhubiri wa injili unapaswa kufahamu kwa faida ya wokovu wako ufahamu wenye dhambi wanakutazama wewe. Usifanye makosa au dhambi ili wasome matendo yako na ya nuru anaweza kusema jinsi nilidhaifu ktk kudhulumu ktk biashara unaweza kufanya biashara bila kudhulumu na ukapata faida.

1) Wasioamini au walioikataa injili unayowabiri(wasiokoka)

**Luk10:16** "**Awasikilizaye** ninyi **anisikiliza** mimi, naye awakataaye ninyi anikataa mimi; naye **anikataaye** mimi amkataa yeye **aliyenituma.** "

2)Wataabishao yataabu za wengine zinakutoa kukufanye uache kufanya kazi ya kuhubiri injili kama wewe ni mhubiri au mtume au nabii na kufanya kazi za kawaida au tabu mfano ujenzi au kilimo kwa mkono au jembe.

**Yohana 4.38** "Mimi naliwatuma myavune yale **msiyoyataabikia**; wengine walitaabika, nanyi mmeingia katika **taabu yao."**

3)Watu wa nyumbani mwako

**Mathayo 10 : 34 — 36** " Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; la! Sikuja kuleta amani, bali upanga. Kwa maana nalikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe mtu; na **adui za mtu** ni wale wa **nyumbani mwake.** "

4) Mapepo(kifafa,kichaa,mchafu,bubu,kiziwi),wakuu wa giza (Wachawi, wakuu wa mila na desturi za kabila,waganga wa kienyeji na miti shamba), falme na mamlaka za giza (serikali na falme za dunia)

# 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**


Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :

**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 35666

Mwenge DSM Tanzania



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034